



MWONGOZO A KUSAHISHA

GRADE 6 – KISWAHILI INSHA (20 ALAMA)

SEHEMU A: INSHA (ALAMA 20)

Siku tuliyoisubiri kwa hamu na ghamu hatimaye ilifika. Ilikuwa siku ya michezo na sote tulikuwa tumejiandaa kwelikweli. Tuliamba mapema asubuhi tukiwa na furaha kubwa na sare zetu za michezo. Walimu walitukumbusha kuhusu nidhamu, ushirikiano na usalama.

Tulipofika uwanjani, kila timu ilijipanga tayari kushindana. Mashindano yalipoanza, shangwe na vigelegele vilijaa kila upande. Nilishiriki katika mbio za mita 100. Nilipoanza kukimbia, moyo wangu ulikuwa na hamasa kubwa. Nilijitahidi sana na mwishowe nilifika mstari wa mwisho nikiwa mshindi wa pili.

Wanafunzi wenzangu walinishangilia na walimu walinipongeza kwa juhudi zangu. Baadaye kulikuwa na michezo mingine kama mpira wa miguu, kuruka kamba na kurusha mkuki. Siku hiyo ilikuwa ya furaha na burudani kubwa kwa kila mwanafunzi.

Mwisho wa siku, mkuu wa shule alitoa zawadi kwa washindi na kututia moyo kuendelea kufanya vizuri. Tulirudi nyumbani tukiwa na furaha na kumbukumbu nzuri za siku hiyo ya michezo.

RUBRIKI YA ALAMA

SEHEMU	VIGEZO	ALAMA
Maudhui (Content)	Uhusiano na mada, ubunifu, na ukamilifu wa hadithi	0 – 8
Mpangilio (Organisation)	Utiririko wa mawazo, aya, utangulizi na hitimisho	0 – 4
Sarufi na Matumizi ya Luga	Matumizi sahihi ya maneno, tahajia na alama za uandishi	0 – 6
Msamiati (Vocabulary)	Utofauti na ufaafu wa maneno	0 – 2

VIWANGO VYA UFAULU

Kiwango	Alama	Maelezo
KUZ	17 – 20	Insha bora, ubunifu mkubwa, makosa machache
KUF	13 – 16	Insha nzuri, makosa madogo
KUK	7 – 12	Mawazo machache, makosa mengi
CHI	0 – 6	Insha dhaifu, haieleweki vizuri